

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**



**WARAKA NA.1 WA MWAKA 2025 KUHUSU MATUMIZI YA**  
**WAVU WA MAKILA (*GILL NETS*) KWENYE ZIWA TANGANYIKA**

*(Chini ya Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Uvuvi, Sura 279)*

2. Serikali, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi), inalo jukumu adhimu, chini ya Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sura 1 (Toleo la 2005) na matakwa ya Sheria ya Uvuvi, Sura 279 (kama ilivyorekebisha), la kusimamia, kulinda, kuhifadhi, na kuendeleza mali asili za nchi (ikiwa ni pamoja na rasilimali asili za uvuvi) inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi. Vile vile, Mkurugenzi wa Uvuvi amepewa mamlaka ya kisheria kutoa Nyaraka na Miongozo mbalimbali kwa kadri ya uhitaji ili kuhakikisha kwamba, rasilimali za uvuvi zinaendelezwa, kusimamiwa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.
3. Kwa sasa kuna changamoto zinazotokana na uvuvi wa kutumia wavu wa makila (*gill net*) wenye macho madogo na usiokuwa na ukomo wa urefu na kina. Hali hii inasababisha wavuvi kuvua kwa wingi samaki wachanga aina ya migebuga na aina nyingine ya samaki wasiokusudiwa. Endapo hakutakuwa na hatua mahsusi, jambo hili litaendelea kusababisha uharibifu wa mazalia ya samaki, makulia na uhifadhi wa mazingira hivyo kuhatarisha uendelevu wa rasilimali za uvuvi hususani samaki jamii ya migebuga katika Ziwa Tanganyika.
4. Hivyo basi, Waraka huu, unaainisha matumizi ya wavu wa makila (*gill nets*) katika shughuli za uvuvi ndani ya Ziwa Tanganyika kama ifuatavyo:-
  - (a) Wavu wa makila (*gill-net*) utakuwa na urefu usiozidi mita mia tatu na thelathini ( $\leq 330\text{m}$ ), idadi ya macho ya nyavu yasiyozidi mia nne ( $\leq 400$ ) kwenda chini (*vertical intergration*), ambapo ni sawa na kina cha maji cha mita ishirini na tano ( $=25\text{m}$ ), na kwamba nyavu zisizozidi furushi tatu (3) zenye jumla ya urefu usiozidi mita elfu moja ( $\leq 1,000\text{m}$ ) kwa kila mtumbwi;
  - (b) Unene wa uzi wa nyavu usiopungua *ply* nne ( $\geq 4$ ) na usiozidi *ply* sita ( $\leq 6$ ) na ukubwa wa jicho la nyavu usiopungua *inch* mbili na nusu ( $\geq 2\frac{1}{2}$ ) au milimita sitini na tatu nukta tano ( $\geq 63.5\text{mm}$ ); na
  - (c) Uvuvi huu utafanyika wakati wa mbalamwezi na katika maji ya kina kirefu kuanzia angalau mita elfu moja ( $\geq 1,000\text{m}$ ) kutoka ufukweni mwa Ziwa Tanganyika.
5. Ifahamike kuwa Waraka huu umetolewa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi, Sura 279 ikisomwa pamoja na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 (na marekebisho yake ya Mwaka 2020 (GN. Na. 492/2020), matakwa ya Ibara ya 6 na ya 7 ya Mkataba wa Makubaliano ya Kikanda ya Nchi Wanachama kwenye Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi katika Ziwa Tanganyika na Bonde lake, uliosainiwa na Nchi Wanachama mnamo wa tarehe 16 Desemba 2021.
6. Inafafanuliwa kuwa Waraka huu utanza kutumika tarehe **7 Aprili 2025** kwenye maeneo yote ya Ziwa Tanganyika na kwamba ukiukwaji wa Waraka huu ni kosa kisheria.

Prof. Mohammed A. Sheikh  
**MKURUGENZI WA UVUVI**